
Department of Motor Vehicles

Kuchapishwa kwenye *New York DMV* (https://dmv.ny.gov)




***SURA YA 6***

# KUPITISHA

### Mada:

- Jinsi ya Kupitisha kwa Upande wa Kushoto
- Jinsi ya Kupitisha kwa Upande wa Kulia
- Kupitishwa
- Mabasi ya Shule
- Maswali ya Sura ya 6

> ***Kumbuka:*** *Maswali ya mazoezi yanapatikana to kwa zile sehemu za kitabu cha mwongozo zinazozungumza sheria za barabara (Sura 4 hadi 11 na Ishara za Barabara).*

Sheria inataka tuendeshe upande wa kulia wa barabara. Tunaporuhusiwa kupitisha magari mengine, kwa kawaida tunayapitisha upande wa kushoto. Unaruhusiwa kupitisha upande wa kulia katika hali fulani tu na inapaswa kufanywa inapohitajika tu na ni salama. Unapopitisha magari mengine au kubadilisha njia ili kuepuka hatari, fanya na uangalifu na inapohitajika tu. Hupaswi kuzidi kikomo cha kasi ili kupitisha gari lingine.

Unapopitisha pikipiki, kumbuka kupa pikipiki upana kamili sawa wa njia kama magari mengine yanaruhusiwa. Usisonge kamwe katika nafasi sawa ya njia kama pikipiki, hata ikiwa njia ni pana na pikipiki iko upande moja.

Unapopitosha baiskeli, hakikisha kumpa mwendesha baiskeli nafasi ya kutosha kuendesha. Unapopitisha mwendesha baiskeli kutoka nyuma, sheria inahitaji umpitishe upande wa kushoto kwa umbali salama mpaka baiskeli imepitishwa.

Sheria inahitaji utumie taa za ishara au ishara za mkono ili kuonyesha nia yako ya kubadilisha njia angalau futi 100 *(30m)* kabla ya utabadilisha njia. Hupaswi kamwe kupitisha gari limelosimama kwenye kivuko kuruhusu mpita njia kuvuka.

## Jinsi ya Kupitisha Upande wa Kushoto

Njia ya kushoto inatumiwa kikawaida kupitisha magari mengine. Huwezi kupitisha gari kwa upande wa kushoto ikiwa:

- Njia yako ina mstari wa njano wa katikati usiokatwa.
- Huwezi kurdui kwa usalama kwa njia ya kulia kabla ya kufika mstari wa njano wa katikati usiokatwa kwa njia ya kulia.
- Huwezi kurudi kwa usalama kwa njia ya kulia kabla ya gari lolote linalokuja linakuja kati ya futi 200 *(60m)* kutoka kwako.
- Unakaribia kona au kilele cha kilima kwenye barabara ya njia mbili na huwezi kuona kuzunguka yake au juu yake.
- Uko kati ya futi 100 *(30m)* ya kivuko cha reli kwenye barabara ya njia mbili.
- Uko kati ya futi 100 *(30m)* ya daraja, handaki au barabara iliyo chini ya ardhi au mfereji wa maji kwenye barabara ya njia mbili na mtazamo wako umezuiwa.

Ikiwa hali zinafaa kupitisha, angalia vioo vyako na ashiria badiliko lako la njia. Kabla ya utaingia njia ya kushoto, angalia haraka juu ya bega lako la kushoto, kupitia dirisha la nyuma ya upande, kuhakikisha hakuna gari karibu nyuma yako katika njia ya kushoto. Usitegemee kamwe vioo vyako unapotayarisha kubadilisha njia. Hata vioo vilivyorekebishwa sahihi vitaacha maeneo yasiyoonekana nyuma ya kila upande wa gari lako. Ikiwa gari liko katika eneo lisiloonekana, huenda hutaliona katika vioo vyako. Sikuzote uangalie haraka juu ya bega lako kabla ya kubadilisha njia au kupitisha.

Unapopitisha, songa kabisa katika njia ya kushoto. Kabla ya utarudi kwa njia ya kulia, ashiria na angalia kwenye kioo chako cha kuona nyuma na hakikisha unaweza kuona bumper ya mbele ya gari ulilopitisha. Angalia haraka juu ya bega lako la kulia kuhakikisha kwamba unaweza kuona angalau futi kadhaa za lami kati ya gari lako na lile ulilopitisha. Kisha rudi kwa njia ya kulia.

## Jinsi ya Kupitisha Upande wa Kushoto

Kikawadia unaweza kupitisha magari mengine kwa upande wa kushoto, hali fulani zinakuruhusu kupitisha kwa upande wa kulia. Unaweza kupitisha gari kwa upande wa kulia tu katika hali zinazooredheshwa chini na tu ikiwa unaweza kupita kwa usalama. Huwezi kuendesha juu ya au kuvuka pembeni au mstari wa makali ya barabara isipokuwa ishara inairuhusu au inaonyehswa na ofisa wa trafiki (ona Sura ya 4 [2]). Unaweza kupitisha kwa upande wa kulia:

- Gari la mbele linapoenda upande wa kushoto.
- Wakati uko kwenye barabara ya njia mbili yenye alama kwa njia mbili au zaidi au ni upana wa kutosha kwa njia mbili au zaidi katika kila mwelekeo, na kupitisha hairuhusiwi na ishara au kukatazwa na magari yaliyoegeshwa au vizuizi vingine.
- Wakati unaendesha kwenye barabara ya njia moja yenye alama kwa njia mbili au zaidi au ni upana wa kutosha kwa njia mbili au zaidi, na kupitisha hairuhusiwi na ishara au kukatazwa na magari yaliyoegeshwa au vizuizi vingine.

Ikiwa utatayarisha to kupitisha upande wa kulia kwenye makutano, angalia magari mbele kwa makini. Hakikisha gari linalokaribia halitayarishi kulielekeza kushoto katika njia yako, na angalia kwenye upande wa kulia wa barabara kwa wapita njia, waendesha baiskeli, watelezaji wa mstari na madereva wa pikipiki ndogo.

Kabla ya utapitisha kwa upande wa kulia kwenye barabara za njia nyingine kama njia za haraka, hakikisha utaangalia vioo vyako, tumia ishara sahihi kwa badiliko la njia na angalia juu ya bega lako la kulia kwa magari mengine. Baada ya umepita, hakikisha kuangalia haraka juu ya bega lako la kushoto na kuashiria kabla ya utarudi kwa njia ya kushoto.

## Kupitishwa

Ikiwa gari lingine linakupitisha kwa upande wa shoto, punguza kasi yako kidogo na baki katikati ya njia yako. Wakati gari limepopita kwa usalama na ni mbele yako, endelea kwa kasi yako ya kawaida.

Ikiwa unaona kwamba unapitishwa kwa upande wa kulia na magari mengi, unapaswa kuingia njia ya kulia na kuwaruhusu kukupitisha kwa upande wa kushoto.

## Mabasi ya Shule

Wakati basi la shule linawasha taa zake za nyekundu, magari yanayokaribia kutoka mwelekeo wowote, hata mbele ya shule na katika mahali pa maegesho pa shule, yanapaswa kusimama kabla ya yatafika basi. Unapaswa kusimama angalau futi 20 (6 m) kutoka kwa basi. Unaweza kutambua basi lile kwa ishara ya "SCHOOL BUS" (BASI LA SHULE), taa za nyekundu juu yake, na rangi yake ya pekee ya njano machungwa.

Kabla ya basi itasimama kupakia au kuwatoa abiria, dereva kikawaida atawasha taa za njano za kuonya zinazopatikana mbele na nyuma ya basi karibu na paa. Unapoziona, punguza kasi na uwe tayari kusimama.

Unaposimama kwa shule la basi, huwezi kuendesha tena mpaka basi linaanza kusonga tena au wakati dereva wa basi au ofisa wa trafiki anaonyesha kwamba unaweza kuendelea. Sheria hii inatumika kwenye barabara zote za Jimbo la New York. Unapaswa kusimama kwa basi la shule hata ikiwa liko upande mwingine wa barabara kuu iliyogawanywa.

Baada ya umesimama kwa basi la shule, angalia kwa watoto wakiwa pembeni ya barabara. Endesha polepole mpaka umewapitisha.

Dokezo la Usalama: Vifo na majeraha vingi vinavyohusishwa na basi vinatokea wakati watoto wanapovuka barabara baada ya kutoka basi, si katika migongano yanayohusisha mabasi ya shule.

Kumbuka kwamba magari yanayosafirisha watu wenye ulemavu yanaweza kuwa na vifaa kama mabasi ya shule na unapaswa kusimama kwao kama ungefanya kwa mabasi mengine ya shule.

Faini unapopitisha basi la shule linalosimama inaanzia kiwango cha chini ya $250 kwa uvunjaji sheri wa kwanza mpaka upeo wa $1,000 kwa uvunjaji sheria tatu katika miaka mitatu. Ikiwa utatiwa hatiani ya tatu za hizi uvanjaji sheria katika miaka miatatu, leseni ya udereva yako itafutwa kwa kiwango cha chini cha miezi sita.

Wamiliki wa Gari - Sheria ilipitishwa mnamo 2019 1 inayoidhini maeneo ya shule na manispaa kutumia kamera za mkono wa kusimamisha kwenye mabasi ya shule kutoa adhabu kwa wamiliki wa magari yanayopitisha basi la shule wakati basi la shule linasimama kwa kusudi la kuwashusha au kuwapandisha abiria na taa za nyekundu kwenye basi la shule zinawaka.

- Uvunjaji sheria wa kwanza - adhabu ya $250
- Uvunjaji sheria wa pili kati ya miezi 18 - adhabu ya $275
- Uvunjaji sheria wa tatu (au zaidi) kati ya miezi 18 - adhabu ya $300

## Maswali

Kabla ya utaenda kwa Sura ya 7, hakikisha unaweza kujibu maswali haya:

- Katika hali nyingi, ni upande gani unaweza kupitisha gari lingine linaloelekea mwelekeo sawa?

- Unapaswa kufanya nini kabla ya kupitisha gari lingine?
- Unapaswa kuona nini katika kioo chako cha kuona nyuma kabla ya ujaribu kurudi kwa njia ya kulia baada ya umepitisha gari kwa upande wa kushoto?
- Katika hali gani unaweza kupitisha gari kwa upande wa kulia?
- Wakati gani unaweza kupitisha gari linalosimama kwenye kivuko kuruhusu mpita njia kuvuka?
- Unapaswa kuchukua hatua gani wakati gari lingine linapokupitisha kwa upande wa kushoto?
- Taa za njano za basi la shule kuwaka na kuzima inamaanisha nini?
- Taa za nyekundu za basi la shule kuwaka na kuzima inamaanisha nini?

**Mwisho wa Sura ya 6:** ✓ Maswali ya Sura ya 6 [1]

< Sura ya 5 [3] | Yaliyomo [4] | Sura ya 7 > [5]

---

1. 1. Unaweza kuona maandishi kamili ya sheria kwenye DHIMA YA MMILIKI KWA KUSHINDWA KWA DEREVA KUSIMAMA KWA BASI LA SHULE LINALOONYESHA ALAMA NYEKUNDU INAYOONEKANA NA MKONO WA KUSIMAMISHA (VTL 1174-A) [6]